JUMATANO

Asubuhi ya Jumatano nilishtushwa kwenye saa kumi hivi za alfajiri na ndoto mbaya kuwa kuna mtu anataka kunibaka. Alikuwa amenivuta kichakani na tulikuwa watu wawili tu hakuna mtu mwingine. Nilijaribu kupiga kelele lakini sauti haikutoka kwenye koo langu. Nilijaribu kujitoa mikononi mwake lakini ndivyo mikono yake ilivyozidi kunishikilia. Mojawapo ya hofu za msingi kabisa za kila mwanamke tangu unapojijua kuwa ni mwanamke ni hii ya kubakwa. Tunaishi na hofu hii, tunatembea nayo na tunalala nayo. Ni hofu kwa namna fulani inahusu kabisa uwepo wetu kama binadamu na mojawapo ya vitu ambavyo vinatufanya wanawake wengi kutokuwa katika hali ya utulivu tunapokutana na mwanamme tusiyemjua au hata tunayemjua katika mazingira ya upweke wa watu wawili tu.

Ndoto ilikuwa ni mbaya hivyo. Mtu huyo alikuwa amenibana mikono yangu nyuma ya kichwa changu ardhini nikiwa nimelala chali. Kwa kutumia miguu yake alikuwa anajitahidi kuichanua miguu yangu ili aweze kujiweka katika nafasi ya kuniingia. Niliweza kuuona uume wake ukiningia katika hali ya utayari wote wa kufanya mauaji. Nilishtuka usingizini na kukuta mume wangu anamalizia kunichojoa chupi yangu. Usingizi ukaniruka ghafla na kabla sijajua anachotaka kufanya alinifungua miguu yangu kwa miguu yake kama ilivyokuwa ndotoni na alikuwa tayari “kuichomeka”.

“Unafanya nini baba Rena?” nilimsukumiza pembeni ya kitanda kwa nguvu kama vile aliyekuwa juu yangu ni jambazi lilitoroka Segerea likiwa na usongo na ukame wa kifungo cha maisha. Nilijisikia kutetemeka. Sijui ni kwanini lakini hata yeye alishtuka mno kwani mara kwa mara akitumia mbinu hiyo nilikuwa nikimtolea nje kwa upole tu au kumbishia kwa kumbania miguu na wakati mwingine nikijisikia kumuonea huruma nilikuwa namtuliza hamu yake kwa kutumia mikono yangu lakini kumpa kabisa. Unajua ni rahisi sana *kuwatuliza* wanaume. Lakini leo haikuwa hivyo.

“Wewe ni mke wangu na haiwezekani ukawa unaninyima unyumba hivi kila siku mama Renata” alikuja juu. Kwa mara ya kwanza hakukubali kushindwa na mimi kirahisi hivyo. Alikuwa amekaa kitandani akiwa uchi wa nyama. Anahema kama mtu aliyefukuzwa na simba na akanusurika. Na mimi nilikuwa na hema kwa sababu zangu. Sikuamini tulikuwa kama chui wawili waliofungwa kwenye chumba kimoja na wakiwa tayari kukwaruzana hadi mshindi apatikane.

“Ndio nikiwa mke wako inamaana uniingie hata kabla sijalowa!?, ukinichanachana je?” nilikuja juu na mimi. Aflajiri hiyo sauti zetu za minong’ono zilikua zinasikika zaidi kuliko tulivyodhania.

“Clementina, ndio nimefanya makosa lakini huwezi kunihukumu milele” alisema kwa hamaki na kwa hasira.

“Ungejua makosa yako ungeyaepuka kabla ya kuyafanya lakini umeendelea na makosa hayo hayo” nilimuambia kwa kiburi tena kwa sauti ya dharau. Sikutaka kumpa uwanja ashinde na zaidi ya yote sikuwa tayari aharibu mpango wangu wa siku hiyo wa kwenda kuomba msamaha kwa kijana Mjamaika. Kwa kawaida watu wakikosa huomba msamaha. Yeye hakutaka

kufanya hivyo ati kwa sababu alikuwa ni “waziri”. Na uwaziri wake aende *huko huko.*

“Clementina mpenzi, naomba unisamehe kweli” alinibembeleza. *Umechelewa.* Aliniomba msamaha akiwa amechelewa mno kwani alitakiwa kuniomba msamaha kabla ya juzi.

Kweli mume wangu alinifanyia makosa ambayo hata wazazi sijapata muda wa kwenda kuwajulisha au kutafuta ushauri wao. Nimeamua kushughulikia jambo hili mimi mwenyewe na litaisha kwa uchaguzi na muda nitakaoamua mimi.

Nilitoka kitandani na kuelekea maliwatoni. Nilikuwa nimeshikwa na donge jingine na kumshangaa mume wangu. Usiku huo kweli alikuwa ni mgeni kabisa machoni kwangu *he was a stranger in my room*. Sikumjua wala sikuamini namjua au kwamba nimewahi kumjua (kwa maana zote za kibiblia na za kimaisha). Nilimuona kama mtu mwingine ambaye alijaribu kunibaka. Akanifanya nikumbuke ile siku ya machozi, siku aliyoniliza mtoto wa watu na kunifanye niape kuwa siwezi kumpenda tena mtu jinsi nilivyompenda yeye.

Bado alikuwa amekaa kwenye ukingo wa kitanda, viwiko vya mikono yake ameviegamiza kwenye magoti yake huku mikono yake mikubwa kama ya mchezaji wa mpira wa vikapu ameishika kichwani akiwa kwenye dimbwi la fikara. Sikumuonea huruma kwa kweli kwani nilijua amejitakia mwenyewe kifungo nilichomuweka.

“Baba Renatus, bado nina mambo ambayo yananisumbua moyoni na mawazoni; sijui nitayamaliza vipi lakini tafadhali sana usijaribu kuniingia kwa nguvu kwani haitatusaidia na itanifanya nitoke kwenye kuwa na kero na wewe na kufika kwenye kuwa na chuki” nilimwambia taratibu nikiwa nimesimama mbele yake na wakati huo nikiwa nimejifunika koti la chumbani nisije nikamuongezea hamasa nikisimama uchi mbele zake maana itakuwa kama panya aliyeshika kiuno mbele ya paka akimpa somo la maadili ya uwindaji.

“Nimekuelewa mpenzi” alisema na kuinuka kwenda bafuni. Miye nilirudi kitandani kumalizia usingizi wangu. Nilijua nusura Waziri aniharibie siku yangu ambayo nilikwisha panga kwenda kumuomba msamaha yule kijana mjamaika. Lakini kitendo chake hicho asubuhi kilinifanya nijiulize maswali mengi; je nilikuwa ninamuadhibu mume wangu kwa ukali mno? Je nikubali kurudisha majeshi nyuma? Je, itakuwaje akiamua kuniacha kabisa? Je kuna siku nitakubali tena anishike, anibusu, anipapase, anitomasetomase na kufanya mapenzi nami nikafurahia kama mara ya kwanza miaka kumi na mitano iliyopita. Nilikosa majibu.

Nilijua tu hata hivyo kuwa endapo nitarudisha majeshi nyuma Waziri anaweza kabisa kurudi na kuendelea na tabia yake ambayo nimeamua kuikataa daima. Niliamua kuendelea na msimamo wangu. Nilijisikia vibaya lakini niliamua liwalo na liwe siyo kosa langu na ni yeye aliyejitakia mwenyewe kuwa kwenye gereza hilo la uchungu na chumba hicho cha kisasi na upweke. Niliamua kulala na kumalizia usingizi wangu nikiwa na kusudio la kuamka baadaye kidogo.

Baada ya kuzama katika lile dimbwi la mapenzi ya kujipa mwenyewe na Mjamaika wangu wa njozini niliamka jioni ile nikiwa mchangamfu kupita kawaida. Na hata baada ya Baba Renatus kurudi aliniacha nikiwa katika hali ya kuchangamka kwani hata kulala nilichelewa nikifanya shughuli mbalimbali za ndani na kwenye ofisi. Nilienda kulala karibu saa saba na nusu za usiku. Sasa kitendo cha kunikatisha usingizi namna ile kilinifanya niwe na unyonge wa aina fulani ambao nilijua utaisha tu endapo nitamalizia usingizi wangu.

Niliombea angalau njozi nyingine ije ya mimi na Mjamaika *wangu*. Usingizi ulipoanza kunichukua nilianza kuota njozi ambayo sikuitaka, njozi ambayo nilikuwa nimeificha mbali na kumbukumbu yangu. Njozi ya miezi saba hivi iliyopita. Njozi ya kunirudisha hadi siku ile ya machozi. Njozi ambayo kwa kweli sikuitaka. Njozi hiyo imekuwa ikinijia kama jinamizi.

* * *

Niliposhtuka ilikuwa saa mbili za asubuhi. Mume wangu alikuwa ameshaondoka kwenda kazini na shughuli mbalimbali zilikuwa zimeshaanza hapo nyumbani na mtaa ulianza kuamka taratibu na kupata uhai mpya kwa siku mpya. Niliamka nikiwa na nia ya kutimiza kabisa dhamira yangu ya kwenda kumtafuta Mjamaika na kumuomba msamaha ili niwe na amani moyoni mwangu na kutuliza akili yangu. Japo nilikuwa nina hamu ya kumjua zaidi na kuona kama anaweza kuniingiza kwenye anga zake hilo hata hivyo halikuwa tumaini kubwa kwani mara nyingi njozi hubakia kuwa njozi tu. Lakini kumuomba msamaha kilikuwa ni kitendo cha kiungwana na kibinadamu ilinipasa kufanya vinginevyo suala hilo lingenisumbua kwa muda mrefu katika moyo wangu.

Nilifanya shughuli mbalimbali za hapo nyumbani na kwenye majira ya saa nne hivi za asubuhi hiyo iliyojaa harufu ya chumvi kwenye anga la Dar nikaanza kujiandaa kwenda tena mjini. Sijawahi kwenda mjini mara mbili ndani ya wiki moja kwa miaka! Sijui nilikuwa nimeingiwa na mdudu gani mwenzenu; ila mdudu huyo kwa kweli hakuwa tayari kuniachia au kunionea huruma.

Kilichonishangaza ni jinsi ambavyo nilihangaika kujua nguo gani nivae kwenda kuomba msamaha. Kwa kawaida mimi nina tofauti na wanawake wengine linapokuja suala la nguo. Ukiniambia tukio basi tayari najua nini cha kuvaa kuanzia kilemba hadi nguo za ndani! Nina nguo nyingi na vidani vya madini mbalimbali na vipodozi ambavyo vingine hata nikitaja huwezi kuamini kwamba vipo hapa Tanzania. Lakini Jumatano hiyo ilikuwa ni kituko. Sikujua cha kuvaa.

Nilikuwa nahangaika niamue kama nivae suruali ya jeans na tshirt tu au blauzi; au, nivae gauni kama mama wa kizungu anayeenda sokoni na kandambili tu bila kuvutia macho ya watu? Sikujua labda ningevaa sketi na blauzi, au kitenge, au kanga. Nilishindwa kuamua kama nahitaji kuvaa kilemba au niende na nywele nimezifunga mabutu. Mwisho katika kuhangaika kwangu huko nilijikuta naanza kucheka. Nilianza kucheka na kwa kweli ilikuwa ni kujicheka mwenyewe. Nilicheka sana hadi nikaa kitandani machozi yananitoka. Sikuamini natafuta nguo ya kwenda kuombea msamaha! Mwenzenu nahitaji kuwekewa mikono au kukemewa! Wengine wanaweza kusema nilihitaji kupepewa!

Ujinga gani huu, niliwaza. Kwani nilikuwa naenda kwenye deti au naenda kwenye mashindano ya urembo? Kilichokuwa kinanipeleka ni kwenda kumuomba mtu msamaha tu na kugeuza zangu, sasa hayo ya kuanza kupiga mahesabu ya nguo, vipodozi, lipsticks na manukato sijui yametoka wapi. Nilipomaliza kujicheka nilikuwa nimefikia uamuzi. Nitatoka katika hali ya wastani bila kuvutia sana hadi watu wadhanie naenda kuomba kazi ya udada poa au kuonekana ndio nimeteremka jana kutoka bara na kiroba changu cha mahindi na kuku mkononi. Wangeniona kama *mwanakijiji* fulani. Niliamua kuvaa sketi nyeusi ya jeans yenye maua maua yaliyochirizwa kwa rangi ya dhahabu kwenye kingo zake chini na tisheti nyeupe na nyepesi ambayo juu yake nilivaa shati la rangi nyeupe vile vile lakini likiwa na michirizi ya maua kwa mbele ikiteremka toka juu kwenda chini na kwenye kola yake vile vile kulikuwa na michirizi iliyorandana na ile iliyo mbele. Vyote vikiwa na rangi ya dhahabu. Nilivaa mkanda kung'ara wa rangi nyekundu. Nilivaa raba nyepesi nyeupe zenye rangi nyekundu kali vile vile.

Nilifunga nywele zangu kwa fundo moja kubwa kwa nyuma na kuzibana kwa kibanio cha rangi kipepeo chenye rangi ya dhahabu. Ni lazima uelewe kuwa nilichanganya damu ya baba Mchaga na mama Muiraqw (wengine wanaita Wambulu) na kwa upande huo wa mama nilijaliwa nywele mwenzenu. Mara kwa mara watu walinifikiria ni Muarabu au Msomali wa aina fulani hivi kwani nywele zangu zilikuwa ni kama shombe hivi nyeusi tii zinazong'ara hata bila ya kutiwa mafuta. Nilipozirudisha nyuma kuzifunga uso wangu ulifunguliwa na kuonesha ukomavu wa umri na uzuri ambao tangu utoto nilisifiwa kuwa ninao. Nyusi zangu zilikuwa zimetengenezwa vyema na zilikuwa kama michirizi myembamba kwenye uso wangu. Nilijua bado wamo, na hakuna mtu ambaye angeweza kunidhania ni mama wa makamo. Kwa kipimo cha haraka mtu angeniona niko kwenye miaka ya mwisho ya ishirini hivi. Sikutaka kujipendezesha lakini baada ya kazi ya kama dakika kumi na tano tu nilijua naweza kutoka. Niliiuma midomo yangu kuhakikisha lipstick inasambaa vizuri na kujipangusa kuhakikisha kuwa sikuonekana kama kinyago huko ninakokwenda au kama mtu aliyetoka kunyonya damu. Nilijipulizia manukato ya *Delices de Cartier by Cartier* niliyopewa kama zawadi na rafiki ya familia yetu tulipoenda Ufaransa mwaka jana. Niliyapenda kwani hayakuwa makali sana na yalikuwa na harufu kama ya maua safi kabisa. *Wamo*.

Niliaga hapo nyumbani kuwa naenda mjini tena na nitarudi baadaye kidogo. Hata hivyo, sikutaka kutumia Mercedes na badala yake niliamua kutumia Toyota Corolla nyeupe. Sikupoteza sana muda nilianza safari ya kuelekea mjini huku kichwani nikijaribu namna mbalimbali ambavyo ningeweza kumuomba msamaha yule kijana nikimuona. Nilipofika tu kwenye njia panda inayounganika na barabara ya Morogoro nilijua nitamuanza vipi kumuomba msamaha.

Kwa kweli nilikuwa nimefikia kilele cha kujiamini, sikuwa naogopa chochote kwani nilishaamua kuwa nitakachofanya ni kumuomba msamaha tu na kugeuza bila kujaribu kutafuta maongezi ya ziada kwani vinginevyo ningejikuta nakaribisha majaribu kwenye ndoa yangu. Lakini zaidi nilifikia uamuzi huo baada ya kufikiria kuwa kijana mzuri namna ile isingewezekana asiwe na mtu wake kwa hiyo mimi ni nani hata niingilie mahusiano hayo. Nilijisikia vibaya kwani kwa wakati

wote huo nilikuwa ninajifikiria mimi tu. Sikutaka kufikiria uwezekano kuwa yule kijana alikuwa ni mme au mchumba wa mtu. Kwa hiyo niliamua kuwa nikifika huko nitamuomba msamaha akikubali au asipokubali lwake lakini mimi nitakuwa na moyo mweupe.

Nilipofika mjini nilitafuta mahali tofauti na pale wizarani kuegesha gari langu. Safari hii hata hivyo haikuwa rahisi. Ukiondoa suala la msongamano katikati ya jiji la Dar kitu kingine kinachonikera kwenda mjini ni hilo la kupata mahali pa kuegesha magari kwa usalama. Sijui wakuu wetu wa jiji na wataalamu wetu wa mji huwa wanafikiria vitu gani. Wametengeneza barabara nyingi na nasikia wana mpango sijui wa kujenga bara bara za kwenda juu kwa juu, hata hivyo kwa wengi wetu mojawapo ya vitu ambavyo tungependa kuviona vinafanywa kwa haraka ni kuweka maeneo ya kuegeshea magari haya mambo ya kunyemeleana hadi mtu atoke kwa kweli yamepitwa na wakati.

Nilipata mahali pa kuegesha karibu nusu maili toka mahali ambapo yule Mjamaika alikuwa na kibanda chake. Nilimlipa kijana mmoja ambaye ameajiriwa na watu wa jengo hilo kuangalia magari ya wateja hapo nje. Nilihakikisha ndani ya gari hakukuwa na kitu chochote ambacho kingeweza kuonekana kutoka nje na kuvutia watu kujaribu kunivunjia vioo. Nilianza kutembea taratibu kuelekea kwa Mjamaika. Kwa vile nilikuwa nimevaa raba basi hata mwendo ulikuwa ni wa staha na nilikuwa naenda kama sitaki kama nahesabu hatua. Sikutaka kutoka jasho kabla sijafika. Moyo ulianza kunidunda.

Nilipokuwa natokea kwenye makutano ya Indira Gandhi na Azikiwe ambapo ipo ile sanamu ya Askari niliweza kuona kutokea nyuma kwa mbali kibanda cha Mjamaika. Niliamua kutembea taratibu zaidi na kuanza kuangalia gia ya kuingilia. Nilipokaribia kile kibanda niliweza kuona shughuli zikiendelea kwenye vibanda vingine vya karibu yake lakini sikuona watu wamesimama mbele ya kibanda hicho. Nilikuwa na wasiwasi labda biashara siyo nzuri sana hasa mida hiyo ya mchana ambapo katikati ya Jiji ni kuwa karibu kila mtu yuko “lunch”. Hiyo haikuwa kawaida hata hivyo kwani mida hiyo ndio biashara hunoga sana mitaa hiyo. Nilikuwa nimevaa miwani ya jua na hivyo kuficha macho yangu hasa yalikuwa yanaangalia nini. Nilipigwa na mshangao nilipofika mbele ya kibanda hicho na kukuta kimefungwa. Hakukuwa na mtu yeyote wala dalili kuwa kulikuwa na mtu siku hiyo. Palikuwa kimya jii.

Kwa sekunde chache sikujua cha kufanya nini. Nikaangaza angaza macho na kuwaona wafanyabiashara wengine wakiendelea na shughuli zao bila kujali kuwa Mjamaika hayupo. Nilianza kuingiwa na wasiwasi na kama mtu ambaye nimemkosa rafiki yangu nikaanza kujiuliza kama amefunga ametoka kidogo atarudi au amefunga mgonjwa kwa hiyo ameshindwa kuja kazini au kitu gani kimemfanya afunge kituo chake cha kazi.

Baada ya kushangaa kwa sekunde chache nilienda kwenye kibanda cha pili kilichokuwa upande wa kulia wa kibanda cha mjamaika. Nilimkuta dada mmoja ambaye alikuwa amejifunga kanga na amevaa tisheti nyeusi na nywele zake amezisuka ile staili ya zamani ya “twende kilioni”.

“Habari yako dada” nilimsalimu kwa heshima baada ya kupisha wateja wawili waliokuwa mbele yangu kumalizia shughuli zao.
Hali ya hewa ilikuwa ni nzuri, jua lilikuwa kali na upepo kutoka bahari ya Hindi ulijaribu kupuliza na kutuliza ukali wa joto la jiji letu hilo. Kwa mbali nilisikia kunguru wakilia kama wanaofurahia kichekesho kinachoendelea hapo chini. Mlio wa magari yaliyokuwa yakipita nyuma yangu kama kwa kupokezana ulikuwa kama kibwagizo cha wimbo usiokuwa na waimbaji. Kelele za wapiga debe wa daladala zilikuwa sikisikika huku wakiitia kwa kugombea wateja “Kinondoni A”, “Msasani”, “Ubungo” na mengine yakilia “Rangi Tatu”. Mengine yalisimama mengine yalipita yakiwa yamejaa watu. Kwa namna fulani nilijisikia raha kuwa niko Dar.

“Nzuri tu dada, habari za mchana?” alinisabahi. Lafudhi yake ilinidokeza kuwa binti huyo alikuwa ni Mpare.
“Naitwa Clementina” nilinyosha mkono na kumsalimia. Nilivua miwani yangu na kuishika mkononi ili kumpa nafasi ya kuyaangalia macho yangu ili asije akadhani najificha kuonana naye.
“Naitwa Rose Msuya” alinijibu huku akipokea mkono wangu kunisabahi na akauchilia.
“Huyu mwenzio hapa yuko wapi kuna vitu nilitaka kununua tai fulani niliziona juzi hapa” nilimwambia nikimdanganya. Ni kweli kulikuwa na tai ambazo nilizipenda na ningependa kumnunulia mume wangu au hata kumpa zawadi kakangu.
“Nani, Freddy?” aliuliza.
“Sijui ndiyo Freddy, ana nywele zakirasta hivi” nilimjibu kwa kumpa taarifa za kumsaidia kumtambua ninaye mzungumzia. Nilicheka ati nilichokiona cha kumtambulisha ni hizo nywele za kirasta. Sijui kwanini sikusema ananizingua kwa lafudhi yake ya kijamaika. Nilijicheka moyoni.
“hahahaha, ndiyo Freddy Mjamaika” alisema na kucheka huku akigeuka nyuma kumpatia mteja mmoja pakti ya sigara aliyokuwa ameilipia. Nilisogea pembeni kupisha. Na mimi nilimuunga mkono kwa kicheko cha kivivu. Hatimaye nilijua jina la Mjamaika wangu. Sijui kama alikuwa ni wa kwangu *peke yangu* hata hivyo.
“Kumbe ni Mjamaika, nilidhani ni hawa marasta wetu wa Bongo” nilisema na mimi na nilichomekea swali la kijanja.
“Hana Ujamaika wowote! Freddy Mluguru huyo ila yuko sana katika mambo ya imani ya majah *people*” alinifafanulia. Kumbe Mjamaika alikuwa ni kijana wa Udzungwa; Mluguru.
“Sasa ndio maana mnamuita Mjamaika” nilisema kama nathibitisha tu alichokisema.
“Ndiyo, lakini yeye mwenyewe anaamini kabisa kuwa marastafari ni wateule wa Mungu, anamuabudu yule Haile Selassie na hasikilizi nyimbo nyingine zozote isipokuwa zenye maudhui ya reggae. Amekariri karibu nyimbo zote za kina Bob Marley, ukimuona anacheza ndio utazimia” alisema na kunipa taarifa hadi zikanifanya nisikie wivu kidogo. Huyu mbona anamjua sana, *na anamjuajuaje*?
“Ah kumbe, sasa alisema anaenda wapi au atarudi lini” niliamua kukatisha mtiririko wa masimulizi ya Rose kabla hajanifanya nimchape vibao kwa kumzungumzia sana hivyo mjamaika *wangu*. Ana haki gani ya kumzungumzia *mpenzi wangu* namna hiyo utadhani anamjua.
“Kusema ukweli dada wala hajaaga, tangu juzi mchana alikuwa mnyonge na ninavyosikia anataka kuhamisha kabisa hiki kibanda kutoka hapa na kukipeleka sijui wapi mwenyewe” alisema.

Moyo ulinishtuka na nilihisi vinyweleo vyangu vikisimama kama vilivyopigwa na ubaridi au kama paka anavyohisi kuna kitu kibaya hujikuta ngozi nzima imesisimka. Sikutaka kuamini kuwa yawezekana mimi nilikuwa sababu ya Mjamaika kutaka kuhama hapo. Niliombea moyoni nisiwe sababu ya hilo. Nisingeishi kwa amani. Tayari nimeshafanya kosa moja sikutaka kuwa sababu ya matokeo ya kosa hilo.

“Duh” niliguna, “sasa ninaweza kumpata wapi” nilimuuliza na sikujua kwanini niliuliza hivyo maana yule dada aliniangalia kwa sekunde chache kushangaa. Bila ya shaka alijiuliza kama tatizo lilikuwa ni bidhaa ninayotaka ningeweza kuipata popote kwanini nilitaka kumtafuta zaidi ya hapo.

“Kwa kweli sijui” alinijibu. Nilijiona ni kama nimegonga mwamba na sina pengine pa kwenda. Nilijihisi kudhulumiwa na zaidi hasa hamu ya kutaka kumuona ilinizidia.

“Unajua dada nilipokuwa hapa juzi nilikuwa nimempa pendekezo la kumsaidia katika mradi wake mmoja na nikasema nitarudi sasa sijui itakuwaje” nilisema na kuongeza uongo juu ya uongo. Sikuwa tayari kushindwa au kukubali kuwa safari yangu ndiyo imefikia ukingoni. Nilijua kabisa kuwa nisingeweza kukomea hapo na kukata tamaa. Yule mdudu bado hakutaka kuniachia. Kama kulikuwa na njama basi sijui kama ni ya shetani au inatoka kwa mbinguni. Vyovyote vile nilimlilia Mungu moyoni mwangu kuwa isiwe mwisho.

“Mmh, kwa kweli sijui ni wapi lakini unaona ule mgahawa pale” alinijibu baada ya kuniangalia machoni na kugundua kuna kitu zaidi na hakutaka kuingilia undani. Alinielekeza kwa kidole chake upande wa pili wa barabara karibu na ofisi za Zain ambapo kulikuwa na mgawaha mmoja.

“Ehe” niliitikia kwa shauku.

“Ukienda pale muulizie Uncle Tall, yeye ni meneja pale. Huyo Tall ndiyo mtu pekee ambaye anaweza kujua jinsi ya kumpata Freddy kwani wanatoka wote Morogoro na mwenyewe Freddy anamheshimu sana kama kakake mkubwa”. Aliniambia. Nilimshuruku na kumuaga kuondoka. Sikutaka niondoke mtupu baada ya kumpotezea muda huo na labda hata kuwafanya wateja wengine wapiti wakidhania nahudumiwa. Niliamua kununua kanga moja nzuri kweli iliyokuwa na maneno yasemayo “*moyo wa kupenda hauna subira*”. Nilimlipa na kuivaa tena miwani yangu na kujiondoa hapo kuelekea ng’ambo ya barabara. Nilimkatia na shilingi elfu tano ya usumbufu wake. Alinishukuru sana.

Kwa mara nyingine tena nilijisikia kama mtu aliyepigwa ndumba nangae. Nilikuwa kama kikaragosi mkononi mwa mchezeshaji na kama roboti aliyetiwa ufunguo na kwenda mbele kwa fahari lakini si kwa amri yake. Nilihisi ndani yangu kuna nguvu inayonisukuma kufanya hivyo, nguvu ambayo ilikuwa ni kama maji ya mto yaendayo kasi yakiupeleka mtumbwi kuelekea ziwani. Na kama jani linavyopeperushwa na upepo wa kiangazi ndivyo nilivyojihisi katika anga hilo la mapenzi. Sikuweza kurudi nyuma, sikuweza kuachilia na sikuweza kukata tamaa. Nilijua ni lazima nifikie mwisho wa hili. Nimeanza kupanda lazima nipalilie hadi mavuno. Kama yatakuwa mazuri au mabaya hilo jingine, kupanda nitapanda kwani mbegu ninazo.

Nilipofika mle ndani kulikuwa na watu wengi kweli kwani ule ulikuwa ni muda wa “lunch”. Nilitafuta sehemu ya kukaa kwenye kona moja na kujibanza kusubiri mhudumu aje. Wakati nasubiri nilikuwa nashangaa kwani sijawahi kuingia

kwenye hivi vihoteli kwa muda mrefu hivi. Msiseme sijui naringa au nyodo; ni kuwa sikuwa na sababu kwa kweli. Lakini kilichonishangaza ni idadi ya watu waliokuwa 'lunch". Hakuna aliyekuwa anaonekana kuwa ana haraka ya kurudi kazini au kuondoka kwenye mgahawa huo. Sijui lunch za bongo zina muda gani lakini kwa ukweli mtu akikuambia anaenda lunch basi ujue ni lunch ya kweli siyo kula na kuwahi kurudi kazini.

Niliagiza chips na soda baridi na nikakaa kusubiri. Baada ya kuletewa vitu hivyo nilianza kula taratibu huku macho yangu yakiangaza upande mmoja na mwingine kuweza kuona huyo Tall ni nani. Kusema ukweli wala haikunichukua muda mrefu kumuona bwana mmoja ambaye alikuwa ni mrefu akitoa maagizo ya hapa na pale kwa walio jikoni, wahudumu na akisimamia mahali pa kupokelea fedha. Nilielewa kwanini walikuwa wanamuita Tall. Alikuwa amevaa shati la rangi ya bluu na tai nyekundu. Kutokana na wembamba wake na ule urefu kwa vile ile tai na ilionekana kama imening'inizwa kwenye mti mwembamba. Nilitamani kucheka.

Nilikaa hapo kwa muda kama wa nusu saa hadi pale nilipoona watu wamepungua kidogo pale kaunta. Nilimuagiza mhudumu kuwa ningependa kuzungumza na meneja mara moja. Yule mhudumu alikuwa na wasiwasi na hakujua kama amefanya kosa katika huduma yake kwangu. Alisita kidogo. Nilimhakikishia kuwa haihusiani na huduma yake kuna jambo tu nilitaka kuzungumza na bosi wake asiwe na wasiwasi. Alinishukuru na kwenda kumuita Uncle Tall.

"Samahani mama umeniita!" nilishtuliwa na sauti nzito ambayo haikuendana kabisa na umbile la Tall. Nilikuwa nimezama katika fikra huku namalizia vipande vichache vya chips vilivyobakia kwenye sahani. Nilichukua napkin na kujipangusa mdomoni taratibu huku rangi ya lipstick yangu ikibakia na kunikumbusha picha iliyoachwa kwenye kitambaa cha Veronica miaka zaidi ya elfu mbili iliyopita.
"Ndiyo Uncle Tall" nilisema kama vile namfahamu na yeye hakujali kwani karibu kila mtu pale alimfahamu kwa jina hilo. Alichukua muda na kuvuta kiti na kukaa. Nilimuangalia na kuamua kwenda moja kwa moja kwenye swali.
"Bwana Tall nimetoka ng'ambo ile" nikamuonesha kiliko kibanda cha Freddy, "na nilikuwa nimekuja kumtafuta Freddy" nilimuambia. Aliniangalia akijaribu mawazoni make kujiuliza mimi ni nani na kwanini nini namtafuta kijana huyo.
"Kwanini unamtafuta Freddy?" aliniuliza kwa sauti kavu huku akionesha kutokujali mimi ni nani. Hivi hajui mimi ni *mke wa waziri?* Nilijiuliza.
"Nitakuambia ukweli" nilianza na kumsimulia tukio la juzi na jinsi gani tangu hiyo juzi nimejisikia vibaya sana na nimekuja makusudi siku hiyo kutaka kumuomba yule kijana msamaha kwani nilijua nimefanya makosa. Machozi kidogo yalinilenga na sikujua kwanini niliamini atanielewa. Kitu pekee ambacho sikumuambia na nisingethubutu kumuambia kuwa mimi ni mke wa waziri.
"Ah, kumbe wewe ndiyo mwanamke *yule*" alisema huku mikono yake kaiweka mezani. Aliniangalia machoni kama mtu aliyepatwa na hasira na kama angekuwa na uwezo angenizaba vibao hapo hapo hadharani. Alishusha sauti yake chini zaidi lakini ikiwa thabiti zaidi.
"Wewe ndio sababu Freddy amefunga kibanda chake pale, na kwa kweli ulivyofanya haikuwa vizuri kabisa." Alizungumza nami kama baba anavyozungumza na binti yake.

Nilijiona mdogo kweli na mnyonge. Uncle Tall hakuangalia uzuri wangu au maumbile yangu. Niliona kwenye kidole chake cha chanda kulikuwa na pete. Hakuwa interested na mimi. Alinizungumzisha kunipa ukweli ambao bila ya shaka alilazimika kuutoa ulivyo. Nilikaa kimya kumsikiliza na sikujaribu kubisha au kujaribu kutoa ufafanuzi. Nusura nimuambie *"you know who Iam?"* sikufanya hivyo. Aliendelea " Freddy alijihisi umemvua nguo hadharani na jioni ile alipokuja kwangu alikuwa amekata tamaa kwani wenzake wote pale walianza kumfanya kuwa ni kituko" alinielezea. Alitumia muda kunifafanulia kwanini Freddy aliamua kubadilisha maskani ya kibanda chake hicho na kuwa japo alikuwa na mpango wa kufanya hivyo kabla ya tukio la juzi jambo hilo lilimfanya aharakishe tu sasa. Nilijisikia ahueni kidogo lakini bado nilijisikia vibaya. Kwa namna fulani nahusika na uamuzi wa Freddy.

"Sasa Tall, nitafanya nini nimuombe msamaha kwani nimekosa amani kabisa na sina namna ya kutetea vitendo vyangu vya juzi" Nilikiri na nusura nianze kuelezea jinsi ambavyo nimetokea kumpenda Freddy Mjamaika na jinsi ambavyo masaa yanavyopita nazidi kuwa na hamu na kiu ya kuwa karibu naye. Sikuthubutu kusema. Nilijizuia kujiachilia hivyo katika wakati huo wa unyonge naudhaifu.
"Sijui niseme nini" alijibu. Aliniomba udhuru mara moja na kuwa atarudi na kuondoka kuelekea kwenye ofisi yake. Aliniacha katika hali ya kuchanganyikiwa na maswali. Je ni kweli ndio nimemharibia maisha kijana wa watu au ndiyo yale yale "yaliyopangwa" tena? Nilimsubiri Tall arudi ili nijue sasa kama ndio kusuka kwenyewe au ndio kunyoa kwani kibinadamu nilishafikia hitimisho. Nilijua hata mbinguni watanisamehe kwani sikubakia nyumbani Kiluvya nalia tu au najilaumu bali nilichukua hatua ya kujitahidi kutafuta upatanisho (labda na mengine). Nilisubiri.

Haikuchukua muda Tall alirudi na kuja kuketi pale akiwa na karatasi mkononi. Alinikabidhi.
"Nimezungumza naye na nimemuambia tu kuwa unamtafuta na mwanzoni hakutaka kabisa kuzungumza na wewe kwani nimemdokeza wewe ni nani" alianza kuniambia. Niliiangalia karatasi hiyo na kuona ndani yake kukiwa na namba ya simu ya Freddy. Tena namba zote mbili ile ya Zain na ya Zantel. Sikuamini kuwa nimepata namba yake nusura niruke ruke kwa furaha na kumshukuru Tall. Kabla sijasema aliendelea.
"Unaonekana ni mtu mwenye utu na sijui nini kilikuingia juzi lakini nimemhakikishia kuwa nimezungumza na wewe mimi mwenyewe na hilo tu ndilo limemfanya akubali kuzungumza nawe; tafadhali usinifanye nijutie uamuzi huu" alimaliza na kuniaga. Nilimshukuru sana na nilimuahidi kuwa sitofanya kitu chochote cha kumfanya ajute. Niliamka kuondoka mahali hapo wakati na yeye alirudi kwenye shughuli zake.

Nilitembea nikiwa nimejaa furaha na hamasa ya aina yake. Nilikuwa kama mtu ambaye ameshinda lotto na mkononi amebeba tiketi zake za mchezo huo akielekea kituo cha kudai malipo yake. Nilienda mjini kumuomba msamaha Mjamaika lakini sikufanikiwa. Hata hivyo niliona nimefanikiwa kiasi kwani sasa nimepata nafasi ya hata kuzungumza naye kwa namna ya chemba zaidi kuliko nilivyotarajia. Nilipofika kwenye gari langu nililikuta liko salama na nikamkatia kijana vijisenti kidogo kwa shukrani na kutia ufunguo na kuanza kurejea nyumbani. Sijui nieleze vipi jinsi nilivyojisikia lakini

maneno kwa kweli yalikuwa hayatoshi kuelezea. Mawazo yangu machafu yakaanza kunijia tena kwa vurugu.

Kwa kweli nilikuwa na hamu ya kufika nyumbani mapema ili niweze kumpigia simu. Niliposhika ukanda wa kuelekea kiluvya baada ya kuachana na vurugu za jiji hasa baada ya kupita Ubungo nilishindwa kujizuia. Sikuweza kusubiri hadi nifike nyumbani. Niliamua nimpigie simu.

Mungu wangu, sijui nini kimeniingia mtoto wa mwenzenu.

Taratibu nilinyanyua simu yangu huko mkono mmoja ukiwa umeshikilia usukani. Nililibana karatasi lenye namba kwenye vidole vyangu na usukani huku mkono wangu wa kushoto ukibonyeza namba hizo. Nilianza 713000688 na kusubiri kuita. Mara nikasikia sauti ikianza kuita kwa mlio wa “One Love, One Heart”. Viganja vyangu vililoa kwa jasho la ghafla.
Mara mtu akapokea.

“Hallow!” Nilisikia sauti ya kiume upande wa pili. Sauti ambayo niliijua ni ya nani yuko nyuma yake kwa uhakika wa asilimia mia moja na moja. Tunaweza kusema kwa asilimia elfu moja! *Mbingu zilifunguka na mara sauti ikasika, “huyu ndiye mpendwa wako uliyempenda”*. Niliona malaika wamesimama wakisubiri kunishangilia. Watakatifu na mitume wakiwa wameinuka kwenye viti vyao vyeupe vya enzi. Hata wale wazee ishirini na wa nne na vile viumbe vinne vyenye uhai alivyoviona Yohana kule Patmo vyote vilisubiri kauli yangu. Na roho za mababu na wazee waliotutangulia wote wakiwa pembezoni wakiniangalia mtoto wao nitasema nini. Kulikuwa na ukimya mbinguni. Hata hivyo mwenzenu midomo yangu ilishindwa kufunguka, koo langu lilikauka kabisa na ulimi wangu uliganda kwenye kinywa changu kama uliotiwa gundi ya mbao. Nilishindwa kujibu. Ujanja wote ulinitoka na kupotea kama njozi ya Alinacha. Na kama ukungu wa alfajiri unapotoweka kwa haraka ndivyo hivyo ujasiri wangu. Nilikuwa dhaifu mbele ya sauti yake.

“Hallow” sauti iliniita tena.

* * *